

Changamoto za Kutafsiri Matini za Kiutamaduni katika Jamii Ulumbi: Mifano kutoka Tafsiri ya Majina katika Matini za Kitalii

Hadija Jilala

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Ikisiri

Makala haya yanahusu changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kwa kutumia mifano ya tafsiri ya majina katika matini za kitalii nchini Tanzania. Jamii ulumbi kama anavyoeleza Msanjila na wenzake ni jamii inayozungumza lugha zaidi ya moja kwa ajili ya mawasiliano na dhima nyingine katika jamii. Kwa hiyo, jamii ulumbi ni jamii ambayo kwayo kuna lugha zaidi ya moja ambazo hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano na shughuli za kila siku. Lugha hizo zinaweza kuwa tofauti katika hadhi na dhima yake ndani ya jamii husika. Lengo la makala haya ni kubainisha changamoto zinazojitokeza katika mchakato wa kutafsiri majina ya kiutamaduni katika jamii ulumbi, kubainisha mchakato wa kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi, na kutoa mapendekezo ya mikakati ya kutafsiri matini za kiutamaduni ili kuhifadhi ujumi wa kisanii na ujumbe uliokusudiwa katika jamii. Makala haya yanaonesha kwamba, majina, maana na ujumbe unaobebwa na majina ya kiutamaduni hueleweka ndani ya jamii mahususi. Kwa hiyo, changamoto za kutafsiri majina yaliyofungamana na utamaduni wa jamii yanatokana na tofauti za kiutamaduni ambazo huibebesha mzigo mzito lugha inayounganisha jamii hizo¹.

Maneno Muhimu: *Tafsiri, Utamaduni, Jamii, Changamoto*

Utangulizi

Msukumo wa kuandika makala haya umetokana na ugunduzi na matokeo ya utafiti wa Jilala (2014) kuhusu Athari za *Kiutamaduni katika Tafsiri* kwa kutumia mifano ya matini za kitalii katika Makumbusho za Tanzania. Katika utafiti huo, mtafiti anajadili kuwa, makumbusho, ni eneo ambalo huhifadhi utamaduni wa jamii ili

¹ Katika muktadha wa Tanzania lugha inayounganisha jamii lugha zingine ni Kiswahili

kuurithisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha, uhifadhi wa utamaduni wa jamii katika makumbusho huwa na lengo la kuutangaza, kuuweka wazi na kuufahamisha utamaduni wa jamii za Tanzania kwa wageni ama watalii ambao hutembelea makumbusho hayo kwa lengo la kujifunza na kujionea utamaduni wa Tanzania. Vilevile, uhifadhi wa utamaduni wa jamii hulenga kuvutia watalii na kukuza utalii wa kiutamaduni.

Vilevile, utafiti wa Jilala (2014) ulijikita katika kuchunguza tafsiri za Kiswahili na Kiingereza. Katika utafiti huo, halikuwa lengo la utafiti kuchunguza changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi lakini matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa, ipo haja ya kufanya utafiti zaidi ili kuchunguza namna ambavyo tafsiri ya matini za kiutamaduni inafanyika katika jamii ulumbi kama Tanzania. Mtafiti alitembelea Makumbusho ambayo yalidhihirisha kuwa yalihifadhi utamaduni wa jamii mbalimbali za Kitanzania; kwa mfano, *Makumbusho ya Kijiji cha Makumbusho na Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni*.

Aidha, majina yanayowakilisha vifaa, nyenzo na amali za jamii za utamaduni wa jamii hizo huwa katika Kiswahili na kutafsiriwa kwa Kiingereza. Utafiti huo uligundua kuwa, 90% ya matini za kiutamaduni zilizopo katika Makumbusho ni *tafsiri ya tafsiri* ambapo maneno ya Kiswahili ni tafsiri ya maneno ya lugha za kijamii kama vile Kingoni, Kisukuma, Kihaya, Kimakonde, Kinyakyusa na Kimasai. Jilala (2014) anahitimisha kuwa, mchakato wa kutafsiri *tafsiri ya tafsiri* hupitia katika hatua tatu ambazo ni hatua ya lugha za kijamii (LC)², hatua ya Kiswahili (LL1) na hatua ya Kiingereza (LL2). Kwa mfano, Jilala (2014:293) anasema kuwa, wakati alipofanya usaili na wafasiri wa matini za kitalii ilielezwa:

Huwa tunakusanya vifaa vya kiutamaduni vya makabila kisha tunawahoji wazawa wa jamii husika ili kupata majina ya vifaa na maana zake za kiishara katika utamaduni husika. Baada ya kufanya hivyo tunatafsiri katika lugha ya Kiswahili na kisha tunatafsiri kwenda katika lugha ya Kiingereza.

Swali la kujiuliza: Ni jinsi gani ujumbe wa matini chanzi huweza kuhifadhiwa katika hatua hizo zote? Kwa maana hiyo, haja ya kuandika makala haya na kufanya uchunguzi wa kina ilionekana ina mashiko zaidi. Lengo lilikuwa ni kufanya uchunguzi wa kina zaidi kuhusu changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi hususan majina. Kama tulivyoona, tamaduni za jamii lugha katika jamii ulumbi huwasilishwa na kuelezewa kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha iliyopata mashiko zaidi ya lugha zingine za

² LC ni lugha lengwa

LL1 lugha lengwa ya kwanza

LL2 ni lugha lengwa ya pili

Kiafrika zilizopo Tanzania. Umuhimu wa makala haya umejikita katika kubaini changamoto zinazojitokeza wakati wa kutafsiri matini za kiutamaduni kutoka lugha za kijamii hadi Kiswahili na kisha Kiingereza. Vilevile, kubaini mkakati unaotumika katika kutafsiri majina yaliyofungamana na utamaduni katika jamii ulumbi na hatimaye kupendekeza mikakati ya kuboresha tafsiri ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi.

Tukirejelea hali ya lugha nchini Tanzania inaonesha kuwa, kuna wanajamii wengi ambao huzungumza lugha tofauti na zenye tamaduni tofauti. Aidha, jamii zote zimeunganishwa na Kiswahili, lugha ambayo hutumika katika shughuli za kitalii na mawasiliano ya kuutambulisha na kuuelezea utamaduni wa Tanzania. Aidha, ili kufanikisha mawasiliano kwa watalii kutoka mataifa mbalimbali, matini zilizo katika Kiswahili hutafsiriwa kwa Kiingereza. Hata hivyo, bado utata unabaki, na swali la kujibiwa ni: Je, tafsiri huwezekanaje katika jamii ulumbi?

Kwa hiyo, tatizo ambalo lilitatiza na kuhamasisha haja ya kuandika makala haya linahusiana na kuchunguza uwezekano wa Kiswahili kutumika kuwasilisha utamaduni wa jamii zaidi ya moja na kwa wakati huo huo kuhifadhi ujumbe wa utamaduni wa jamii hizo. Kwa hiyo, lengo la makala haya ni kubainisha changamoto zinazojitokeza katika mchakato wa kutafsiri majina yaliyofungamana na utamaduni wa jamii katika jamii ulumbi. Ili kulifikia lengo hilo, makala haya yanajibu maswali yafuatayo: Ni changamoto zipi zinakabili mchakato wa kutafsiri majina ya kiutamaduni katika jamii ulumbi? Je, ni mkakati upi unatumika katika kutafsiri majina yaliyofungamana na utamaduni katika jamii ulumbi? Na; je, nini kifanyike ili kuwepo na ulinganifu wa ujumbe wa matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi?

Lugha za Tanzania na Majina

Katika nchi ya Tanzania, kuna lugha za kijamii zaidi ya 150 ambazo huzungumzwa katika mikoa ya Tanzania (LOT, 2009). Aidha, kila mkoa wa Tanzania una angalau kabila moja linalotawala. Kwa mfano, tukiangazia mkoa wa Mwanza, lugha inayozungumzwa na wakazi wa mkoa huo ni Kisukuma. Lugha hii inazungumzwa katika wilaya zake zote isipokuwa Ukerewe ambako wanaishi Wakerewe na Wakara ambao huzungumza lugha ya Kikerewe na (ama) Kikara. Aidha, kundi hili la Wasukuma linapatikana katika mkoa wa Shinyanga ambapo kuna kabila dogo la Wanyantuzu waishio wilaya ya Bariadi.

Katika mkoa wa Tabora kuna kabila la Wanyamwezi ambao wanazungumza lugha ya Kinyamwezi, Dodoma kuna Wagogo ambao wanazungumza Kigogo. Hii ikiwa ni baadhi ya mifano inayodhihirisha kuwa Tanzania ina makabila mengi na aghalabu jamii zilizopo katika mikoa hiyo huzungumza lugha tofauti na mkoa mwingine. Tofauti hizi za kijamii, si katika lugha tu, bali pia katika tamaduni na falsafa zao. Hii ikiwa na maana kwamba, kila jamii inaongozwa na mila, desturi, imani, kaida na uzoefu tofauti na jamii nyingine. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa tofauti hizi zinaweza kujidhihirisha katika ugawaji wa majina na maana zinazoashiriwa na

majina hayo ndani ya jamii husika. Kwa mfano, Rubanza (2000) anasema majina ya jamii ya Wahaya yana maana zinazotokana na mazingira ya kuzaliwa, kuongezeka kwa familia, msugvano wa kifamilia na mgongano au mzozano wa kijamii kwa ujumla. Mawazo hayo pia yanajengwa na Rugemalira (2005) ambaye anatoa mifano inayoshadidia kuwa majina ya Wanyambo yana maumbo yanayobainisha maana katika jamii. Kwa mfano, 'nya' na 'ru' yana maana ya 'kuwa na kitu' au 'kumiliki kitu'. Sanjari na mawazo haya, Manyasa (2008) katika utafiti wake wa majina katika jamii ya Wasukuma alibaini kuwa majina hayatumiki katika ombwe bali huhusisha utamaduni wa jamii. Kwa upande mwingine, Msanjila na wenzake (2009) wanasema, maana zitokanazo na majina ya asili huwa na uhusiano na utamaduni wa mzungumzaji, mazingira ya jamii ilipo, majira ya mwaka, matukio muhimu katika jamii husika. Kwa mfano, Msanjila na wenzake (2009:52) wanatoa mifano ifuatayo:

| Jina | Maana |
|-------------------------|--|
| Matonya au Nhonya (-me) | amezaliwa wakati wa mvua inanyesha |
| Mamvula (-ke) | amezaliwa wakati mvua inanyesha |
| Manzala (-ke) | amezaliwa wakati wa njaa, watu wakiwa hawana chakula |
| Mazengo (-me) | amezaliwa wakati wa kukata miti ya kujengea nyumba |

Ukichunguza mifano iliyotolewa na Msanjila na wenzake (wamekwishatajwa) tunabaini kuwa jamii hutoa majina kulingana na utamaduni wa jamii. Swali la kujiuliza: Ni jinsi gani dhana za kiutamaduni zinaweza kuhamishiwa katika utamaduni wa jamii nyingine?

Kwa ujumla, jamii lugha hizo hutofautiana katika misingi ya majina, vyakula, vinywaji, imani na falsafa. Hali kadhalika, tofauti hizo hujibainisha katika namna wanavyotumia imani na falsafa ya kijamii kama utambulisho wao. Kwa mfano, kinywaji cha jamii ya Wahehe ni '*ulanzi*' ambacho huandaliwa kwa namna ya kipekee na huitambulisha jamii hiyo. Hii ni tofauti na jamii ya Wachaga ambao hutumia '*mbege*'. Mtu akitaja '*mbege*' huashiria sifa bainifu inayowatambulisha na kuwatofautisha Wachaga na jamii nyingine za Kitanzania. Sifa bainifu za vinywaji huzitofautisha pia jamii nyingine kama vile; Wafipa '*kimpumu*', Wahaya '*lubisi*' na Wasukuma '*wanzuki*'.

Kama tulivyoeleza hapo awali, hali ya lugha nchini Tanzania inadhihirisha kuwa, pamoja na kuwepo kwa lugha nyingi, jamii zote hizo huwasilishwa na lugha moja kuu; yaani Kiswahili. Ni lugha inayotumika kuunganisha jamii lugha zote. Vilevile, ni lugha ya mawasiliano ambayo kwayo jamii zote huweza kuwasiliana, kusikilizana na kuishi pamoja kama jamii moja. Kiswahili ni lugha yenye hadhi kubwa nchini Tanzania na imepewa hadhi ya kuwa lugha ya Taifa na lugha ya mawasiliano katika shughuli za kielimu, kiuchumi, kibiashara, kisiasa na kijamii. Vilevile, Kiswahili ni lugha inayotambulisha utaifa na utamaduni wa kitaifa ndani

na nje ya nchi. Ni lugha inayounganisha makabila yote ya jamii za Tanzania yanayozungumza lugha tofauti na kuleta umoja wa kitaifa. Hii ina maana kwamba, lugha ya Kiswahili inawaunganisha Wasukuma na Wachaga wakaweza kuwasiliana, kuhusiana, kufanya shughuli za biashara, uchumi na maendeleo ya nchi kwa pamoja. Kwa jinsi hiyo, Kiswahili ni kielelezo cha utamaduni wa Watanzania na kitambulisho cha utifa.

Pamoja na kuwa Kiswahili ni lugha inayotambulisha utifa na utamaduni wa kitaifa ndani na nje ya nchi, Kiswahili kwa jamii ya Tanzania ni lugha ya pili ambapo lugha za Kienyeji huwa ni lugha za awali kwa Watanzania walio wengi. Lugha ya Kiswahili huwa ni lugha ya kwanza ama ya pili inayozungumzwa na 97% ya Watanzania (Msanjila, 1997). Vilevile, lugha ya Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na jamii za Afrika Mashariki kama vile Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Kongo. Ni miongoni mwa lugha kuu duniani inayotumika katika mawasiliano kwenye baadhi ya mikutano ya Umoja wa Afrika (African Union - AU) sambamba na lugha nyingine kama vile lugha za Kiingereza, Kifarasa, Kireno na Kiarabu. Vilevile, Kiswahili ni lugha ambayo inaunganisha nchi za Afrika Mashariki.

Nafasi ya Kiswahili dhidi ya Lugha Nyingine za Kijamii

Lugha ni amali ya jamii inayoizungumza na hubadilika kutegemea vipengele vifuatavyo; siasa, biashara, dini na utamaduni. Sewangi (2004) anadai kuwa, mabadiliko ya jamii yanaweza kusababisha ama kuimarika au kuvia kwa lugha. Kwa mfano, kuimarika kwa matumizi ya Kiswahili Tanzania ni mabadiliko yaliyosababisha kuvia kwa baadhi ya lugha za kienyeji. Moja ya sababu iliyoifanya lugha ya Kiswahili kudhibiti lugha nyingine nchini Tanzania ni kupanuka kwa wigo wake wa matumizi katika jamii.

Kihistoria, Kiswahili ni lugha ambayo ilitumika katika harakati za kudai uhuru pamoja na kuwaunganisha Watanganyika ili kuwafanya kuwa kitu kimoja. Akielezea sifa ya Kiswahili, Ryanga (2004) anasema kuwa ni lugha ya upole, ushawishi, ufahamu wa hadhira na matini. Utaifa wa lugha ya Kiswahili umeifanya iwe lugha inayowasilisha utamaduni wa jamii fulani. Kwa maana hiyo, Kiswahili kinatumika kama njia ya kuelezea utamaduni wa makabila mengine nchini Tanzania. Pamoja na kuwepo kwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya kitaifa, bado makabila mengine yameendelea kudumisha lugha zao, tamaduni zao, mila, kaida na desturi zao ambazo huwatambulisha na kuwatofautisha kama jamii. Katika mkabala huo, ipo haja ya kufanya uchunguzi wa kina ili kuona ni changamoto zipi zinazoikabili tafsiri ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kama Tanzania.

Nadharia ya Utafiti

Uchunguzi na uchambuzi wa data za makala haya, umetumia Nadharia ya Skopos iliyoasisiwa na Hans. J. Vermeer katika miaka ya 1970 kule Ujerumani. Msingi wa nadharia ya Skopos ni kuiona tafsiri kama utekelezaji wa vitendo kwa kuzingatia matini asilia. Ni nadharia ambayo ilileta mageuzi ya mtazamo uliokuwepo wa

kuiona tafsiri kama tendo la kiisimu na hivyo kuitazama nadharia ya tafsiri kama dhana ya dhima na utamaduni wa jamii. Uhamishaji huu wa mtazamo wa tafsiri ulitokana na hamasa ya nadharia ya mawasiliano, vitendo, isimu matini, nadharia ya matini na pia kutoka mikabala ya kifasihi kwenda kwenye nadharia za upokezi (Iser, 1978).

Nadharia hii inasisitiza kuwa, muktadha unaoizunguka tafsiri hauwezi kupuuzwa bali huzingatiwa katika tafsiri. Muktadha huhusisha mambo kama vile: utamaduni wa hadhira, hadhira, wateja na dhima ya matini iliyokusudiwa kwa hadhira ya utamaduni lengwa (Vermeer, 1989). Katika nadharia hii, tafsiri inatazamwa siyo tu kama mchakato wa uhawilishaji, bali pia kama muundo mahususi wa tendo la kibinadamu, ambao ni sawa na matendo mengine ya kibinadamu. Vermeer (1984) kama anavyonukuliwa na Nord (1997) anasema kuwa, kila matini huzalishwa kwa lengo fulani maalumu na lazima ikidhi lengo hilo. Kwa maana hiyo, lengo la tafsiri lazima lielezwe na liwekwe wazi kabla mfaisiri hajaanza kutafsiri. Nadharia hii inasisitiza kuwa, kila tendo lina matokeo yake (Vermeer, 1989, 1999 na 2000, Reiss na Vermeer, 1994). Vermeer (1989) anaeleza kwamba, kanuni ya jumla ya Nadharia ya Skopos ni lengo la matini lengwa ambalo ndilo huukilia mbinu ya tafsiri. Kutokana na kanuni hiyo ya jumla Vermeer aliunda kanuni mahususi inayosema tendo la binadamu (mbadala wake tafsiri) huukiliwa na lengo lake (Skopos) na dhima ya lengo lake.

Vermeer (1989) anaeleza kuwa, tafsiri huzalishwa kwa ajili ya hadhira mahususi, kwa lengo mahususi na katika muktadha maalumu. Nadharia hii imejikita katika kutathmini matini kwa kuzingatia malengo maalumu yanayowasilisha dhima sawa baina ya utamaduni chanzi na utamaduni lengwa. Kwa ujumla, nadharia hii imejikita katika malengo ya tafsiri ambayo huukilia mbinu na mikakati ya tafsiri inayotumika katika kutoa matokeo stahiki ya kidhima. Katika nadharia hii, Vermeer (1987) anazingatia zaidi mpokezi wa tafsiri kuliko chanzo cha makala, kiasi kwamba anaelezea kitendo cha kutafsiri kama kuiwasilisha matini kwa muktadha lengwa, nia lengwa na hadhira lengwa katika mazingira lengwa. Kulingana na mkabala huu, tafsiri nzuri ni ile inayoruhusu hadhira lengwa kupata tafsiri yenye ushikamani na matini chanzi (Nord, 1991a na 2005; Reiss na Vermeer, 1994; Vermeer, 2000; Lauscher, 2000). Aidha, nadharia hii inaakisi uhamishaji jumla wa kaida za kiisimu katika dhana ya tafsiri iliyojikita zaidi kwenye dhima na utamaduni-jamii (Gentzler, 2001).

Nadharia ya Skopos ina kanuni sita, lakini katika muktadha wa makala haya tutajadili kanuni mbili ambazo ni: *kanuni ya ushikamani* na *kanuni ya uaminifu*. Kanuni ya ushikamani humaanisha kwamba, ni lazima matini lengwa iwe na maana kwa hadhira lengwa na katika muktadha wa kimawasiliano ambao matini lengwa itatumika. Kanuni hii inadai kuwa, matini lengwa lazima iwe na ushikamani wa kutosha, na kuwaruhusu watumiaji lengwa kuelewa kwa kutumia maarifa yao ya awali na hali ya mazingira. Matini chanzi, inapaswa kutafsiriwa kwa lugha lengwa kiasi ambacho inakuwa sehemu ya ulimwengu ambao inaweza kutafsiriwa na

hadhira kama ushikamani wa hali yao. Kwa upande mwingine, kanuni ya uaminifu inarejelea ushikamano wa kimatini baina ya matini lengwa na matini chanzi. Hata hivyo, umbo na kiwango cha usahihi hutegemea lengo la matini lengwa na ufahamu alionao mfasiri juu ya matini chanzi. Kwa hiyo, kwa kutumia kanuni hizi tutaweza kuona ni jinsi gani ushikamani na uaminifu unafikiwa wakati wa kutafsiri majina ya kiutamaduni katika jamii ulumbi.

Nadharia ya Skopos imejikita katika vipengele ambavyo ni mahususi katika utamaduni na lugha ya mtu binafsi kama sababu zinazokulia mchakato wa tafsiri. Ni nadharia inayoitazama matini kama nyenzo ya kutolea taarifa iliyoandaliwa na mzalishaji kwa ajili ya hadhira. Kwa hiyo, sifa ya tafsiri ni kutoa taarifa kwa hadhira kwa kutumia lugha ya watu wenye utamaduni na lugha moja (lugha na utamaduni lengwa). Taarifa hizi huwa zimetolewa kwa lugha nyingine ndani ya utamaduni mwingine (lugha na utamaduni chanzi). Pili, mfasiri ni mtoa taarifa. Yaani, mfasiri hutoa taarifa kwa kuiga mtoaji taarifa wa awali. Tafsiri kulingana na Nadharia ya Skopos, huukiliwa na mahitaji na matarajio ya hadhira ya matini lengwa (Vermeer, 1999 na 2000).

Makala haya basi, yanatumia nadharia ya Skopos kuchunguza, kuchambua na kujadili data na matokeo ya data. Kama inavyosisitiza nadharia ya Skopos, tendo la tafsiri huukiliwa na *Skopos* yake, hii ina maana kwamba, mfasiri anapotafsiri, lengo la tafsiri ndilo humuongoza katika kuteua mbinu atakayoitumia katika kutafsiri matini husika. Akisisitiza wazo hili, Nord (2001: 29) anasema, “tendo la tafsiri huukiliwa na ‘Skopos’ yake; kwamba mwisho huhalalisha njia”.

Mbinu za Utafiti

Data za makala haya zilikusanywa katika: Makumbusho ya Taifa na Nyumba ya Utamaduni (Dar es salaam), Kijiji cha Makumbusho (Dar es salaama) na Makumbusho ya Mwalimu J. K. Nyerere yaliyopo Butiama mkoa wa Mara. Vilevile, data zilizokusanywa na Jilala (2014) zimetumika kujaziliza, kujenga na kuendeleza mjadala wa makala haya. Aidha, data za makala haya zilikusanywa kwa kutumia mbinu tatu ambazo ni: *Mbinu ya usomaji wa machapisho*; *Mbinu ya dodoso* na *Mbinu ya usaili*. Walengwa walioshiriki katika kutoa data za makala haya ni wafasiri wa matini za kitalii, wahifadhi mila na waongozaji wa watalii ambao walifanyiwa usaili na kupatiwa dodoso.

Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Makala haya yalilenga kuchunguza changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kwa kutumia mifano ya tafsiri ya majina. Lengo lilikuwa kubaini changamoto wanazokumbana nazo wafasiri wa matini za kitalii wakati wa kutafsiri matini za kiutamaduni hususan majina. Aidha, data za makala haya zimedhihirisha kuwa kuna majina ya aina mbalimbali kama vile: watu, maeneo na mahali, majina ya lugha za kijamii, majina ya utambulisho wa jamii, majina ya vyakula, majina ya mahusiano ya kifamilia, na majina ya vinywaji. Sehemu hii

inawasilisha matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu kulingana na malengo ya makala.

Changamoto za Kutafsiri Majina ya Kiutamaduni katika Jamii Ulumbi

Moja ya malengo mahususi ya makala haya ilikuwa ni kubaini changamoto za kutafsiri majina ya kiutamaduni katika jamii ulumbi. Baada ya kusoma, kuchunguza na kuchambua matini za kitalii data zimedhihirisha kuwepo kwa changamoto ambazo humkabili mfasiri katika mchakato wa kutafsiri majina katika jamii ulumbi. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na: changamoto za kisemantiki, muingilianotamaduni, ukosefu wa visawe vya Kiswahili, tofauti ya dhima ya maneno ya kiutamaduni, tofauti ya tafsiri ya malimwengu, matumizi ya neno moja kurejelea maneno zaidi ya moja na eneo la jamii ulumbi kuwa kikwazo cha mawasiliano. Sehemu ifuatayo inajadili changamoto hizo kwa kutumia mifano kutoka kwa matini za kitalii.

Changamoto za Kisemantiki

Data za makala haya zimedhihirisha kuwepo kwa changamoto ya kisemantiki katika tafsiri ya majina yaliyofungamana na utamaduni. Changamoto hii huhusisha matatizo ya uhawilishaji wa maana kutoka katika matini chanzi kwenda katika matini lengwa. Kila jamii huteua neno na kulipa maana kulingana na makubaliano na falsafa ya jamii husika (Rubanza 2000; Rugemalira, 2005; Manyasa, 2008). Kwa maana hiyo, baadhi ya maneno yanatokea kuwa na maana katika lugha moja na kuwa na maana tofauti katika jamii nyingine. Majina hueleweka ndani ya jamii mahususi, jina linaweza kutumika katika jamii moja na lisitumike katika jamii nyingine, ama kwa maana moja au tofauti na kwa dhima moja ama dhima tofauti.

Baker (1992) anafafanua kuwa, neno la lugha chanzi linaweza kuelezea dhana ambayo haijulikani katika lugha lengwa. Neno hilo linaweza kuwa dhahania au halisi; linaweza kuwa la imani ya kidini, mila za kijamii au aina ya chakula. Hivyo, katika kutafsiri majina yaliyofungamana na utamaduni katika jamii ulumbi huwa vigumu kutafsiri majina hayo kutoka lugha za kijamii kwenda katika Kiswahili kwa sababu majina hayo yamefungamana na utamaduni mahususi. Kwa hiyo, tofauti za kiutamaduni katika jamii ulumbi huathiri tafsiri ya majina na kupoteza maana na ujumbe uliokusudiwa na jina hilo. Maana za matini za kiutamaduni hueleweka ndani ya utamaduni husika na ni vigumu kuwasilisha maana, uamilifu na dhima hizo kwa hadhira ya utamaduni mwingine kwa kutumia tafsiri (Jilala, 2014). Changamoto za kisemantiki hujidhihirisha katika nyanja tano ambazo ni: kupotea kwa maana, upanuzi wa maana, utata wa maana, upotoshaji wa maana na ufinyu wa maana (Jilala, 2014a na 2014b).

Jilala (2014) anadai kuwa, uelewa, upokezi na utambuzi wa maana na ujumbe wa matini hutofautiana baina ya mtu na mtu, na jamii na jamii. Hoja hii inaenda sambamba na mawazo ya Katani (2004) ambaye katika kubainisha matatizo yanayotokana na kutafsiri maana ameyagawa matatizo hayo katika nyanja kuu mbili: kwanza, maana haijengwi bali hutafsiriwa kulingana na mtu binafsi na imani

muambatano ya utamaduni. Pili, maana hujengwa katika muktadha wa kijamii. Hivyo, maana hujikita katika uelewa wa mtu binafsi na namna jamii inavyotafsiri maana ya neno husika. Tafsiri ya maana ya maneno hutofautiana kutoka jamii moja hadi jamii nyingine. Tofauti hizi hutegemea muktadha, wakati, historia na utamaduni (Nida, 2001; Ndlovu, 2000; Jilala, 2014).

Upotoshaji wa maana za Majina

Upotoshaji wa maana ni kitendo cha kubomoa maana ya awali iliyokusudiwa na kuibua maana mpya kwa kuteua visawe tofauti. Upotoshaji wa maana hujitokeza pale mfasiri anapoteua visawe vya lugha lengwa ambavyo vina maana inayokinzana na neno la lugha chanzi. Kwa hiyo, upotoshaji wa maana hujitokeza pale panapotokea ukinzani wa maana baina ya matini chanzi na matini lengwa. Hii ina maana kwamba, neno A linakuwa na maana B. Changamoto hii ilibainika kujitokeza katika tafsiri ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi. Kwa mfano, tafsiri ya majina yanayowakilisha vinywaji, kama tulivyojadili hapo awali kuwa kila jamii ina vinywaji vyake na vinywaji hivyo huwa ni moja ya sifa bainifu za jamii husika.

Vinywaji hivyo hutumika kwa dhima maalumu katika jamii. Changamoto ya kutafsiri majina ya vinywaji hivyo inajidhihirisha katika matini za kitalii ambapo majina yote yanatafsiriwa kwa kuhamishwa kama yalivyo kutoka lugha za kienyeji hadi Kiswahili na hatimaye yanapotafsiriwa kwa Kiingereza hutafsiriwa kwa kutumia kisawe kimoja jumuishi. Tafsiri hii husababisha kupotea kwa maana asilia na kuondoa ushikamani wa maana na ujumbe kati ya lugha chanzi na lengwa. Tazama mifano ifuatayo:

Jewali Na. 1: Tafsiri ya Majina ya Vinywaji

| MC ³ | ML 1 | ML 2 |
|-----------------|---------|-------------------|
| Lubisi | Lubisi | <i>Local bear</i> |
| Mbege | Mbege | <i>Local bear</i> |
| Wanzuki | Wanzuki | <i>Local bear</i> |

Chanzo: Matini za Kitalii za Makumbusho

Mifano katika jedwali Na. 1 hapo juu, inadhihirisha mifano ya tafsiri ya majina ya vinywaji ambapo jina huhamishwa kama lilivyo kutoka lugha ya kijamii kwenda Kiswahili na hatimaye Kiingereza. Hata hivyo, kutafsiri majina ya vinywaji hivyo

³ MC ni matini chanzi (Lugha za kijamii)

ML 1 ni matini lengwa (Kiswahili)

ML 2 ni matini lengwa (Kiingereza)

kwa kutumia neno jumuishi hupotosha maana kwa sababu ‘Lubisi’ haina dhima sawa na ‘Wanzuki’ na wala ‘mbege’ (Jilala, 2014).

Ukosefu wa Visawe vya Kiswahili

Ukosefu wa visawe vya Kiswahili vinavyorejelea majina ya lugha za kijamii ni changamoto inayoikabili tafsiri ya majina ya kiutamaduni katika jamii ulumbi. Data zilizidhihirisha kuwa, lugha ya Kiswahili haina visawe mwafaka vya kurejelea maneno ya lugha za kijamii. Hii ni kwa sababu, pamoja na kuwa zote ni lugha za kibantu, zinatofautiana katika utamaduni na falsafa ya jamii hizo, uelewa na utambuzi wa mazingira ya jamii hizo. Kwa mfano, maneno ya Kizanaki ‘esyo’, ‘mukyero’, ‘ruseke’, ‘obutale’ na ‘ekiranya’ maneno haya yametafsiriwa kama yalivyo katika matini za kitalii. Hii inaonesha kuwa, mfasiri alikosa kisawe cha maneno hayo katika lugha ya Kiswahili na hivyo kuyahamisha kama yalivyo kutoka Kizanaki kwenda Kiswahili na hatimaye Kiingereza. Tatizo la kukosa kisawe humfanya mfasiri ahamishe neno kama lilivyo kutoka katika lugha ya kijamii kwenda lugha ya Kiswahili na hatimaye lugha ya Kiingereza. Kwa kufanya hivi, neno la kijamii hupoteza maana na ujumbe asilia. Kwa mfano, maneno ya hayo ya Kizanaki yana maana na dhima zake ambazo hutambulika ndani ya jamii ya Wazanaki pekee. Maana na dhima hizo hazijitokezi katika matini lengwa na hivyo hueleweka kwa hadhira chanzi tu, na hadhira lengwa huwa haiwezi kupata maana na dhima lengwa. Tazama mifano dhima za maneno hayo katika mifano ifuatayo:

| Neno | Maana⁴ |
|---------------|---|
| i) Esyo | Jiwe dogo linalotumika kusaga nafaka. |
| ii) Mukyero | Mzee ambaye amefikia daraja la juu la heshima. Huruhusiwa kuingia katika sherehe hata za wanawake. |
| iii) Ruseke | Mrija unaotumika na jamii ya Wazanaki kunywa pombe ya asili), |
| iv) ‘Obutale’ | Jiwe kubwa ambalo nafaka husagiwa kwalo |
| v) ‘Ekiranya’ | Kifaa kinachotumika kuhifadhia mirija ya kunywa pombe aina ya amarwa (ulezi na mahindi au ulezi peke yake). |

Mifano hapo juu inadhihirisha kuwa maneno ya Kizanaki yana dhima zake ambazo hazijitokezi katika tafsiri. Kwa hiyo, kuhamisha maneno kama yalivyo kutoka lugha ya kijamii kwenda Kiswahili na kisha Kiingereza husababisha tatizo la mawasiliano baina ya hadhira. Tatizo la mawasiliano baina ya hadhira, haliathiri

⁴ Maana na dhima za majina ya Kizanaki ni kwa mujibu wa Wahifadhi mila katika Makumbusho

watalii wanaotoka nje ya nchi tu bali hata watalii wa ndani hushindwa kupata ujumbe wa matini za kiutamaduni ambazo si za jamii yao. Kwa mfano, Mgogo ambaye ni mwenyeji wa Dodoma na asiyelewa Kizanaki hawezi kuelewa maana na ujumbe wa maneno hayo. Tatizo hili lilimpata pia mtafiti mwenyewe ambaye hana usuli wala ufahamu wa lugha ya jamii ya Wazanaki.

Mtafiti alishindwa kufahamu na kupata maana na ujumbe wa maneno hayo hadi alipopata ufafanuzi kutoka kwa waongozaji wa watalii. Vilevile, mtafiti alishuhudia baadhi ya watalii wa ndani (watalii wa Tanzania) wakishindwa kubaini maana na ujumbe wa maneno hayo. Hii inadhahirisha kuwa, uelewa wa dhana za kiutamaduni hujikita ndani ya jamii husika. Kwa maana hiyo, maneno haya yalitakiwa kutolewa ufafanuzi wa ziada kuhusu maana inayoashiriwa na maneno hayo katika jamii hiyo.

Tofauti ya Dhima ya Maneno ya Kiutamaduni

Tofauti ya dhima ya maneno ya kiutamaduni hutokana na neno moja la jamii fulani kuwa na maana na dhima tofauti na jinsi neno hilo linavyotumika katika jamii nyingine. Kuwepo kwa maneno hayo, husababisha matatizo ya tafsiri hasa pale mfasiri anapokuwa hana maarifa ya utamaduni chanzi. Maneno katika jamii hupewa dhima tofauti kulingana na utamaduni, muktadha, uelewa na uzoefu wa jamii husika. Hii ina maana kwamba, katika jamii za Tanzania kila neno au kifaa hupewa maana na dhima mbalimbali kutegemea muktadha wa jamii inayorejelewa. Kwa jinsi hiyo, neno linaweza kuwa na maana na dhima moja katika Kiswahili lakini katika lugha za kijamii likawa na dhima nyingine tofauti. Tazama mifano ifuatayo:

Jedwali Na. 2: Tofauti ya Dhima ya Maneno ya Kiutamaduni

| MUC | MUL |
|------------|------------------------|
| Kigoda | <i>Royal stool</i> |
| Upawa | <i>Wooden spoon</i> |
| Kiroto | <i>Drinking basket</i> |
| Mtungi | <i>Storage pot</i> |
| Bakora | <i>Stick</i> |

Chanzo: Matini za Kitalii za Makumbusho

Mifano katika Jedwali Na. 2 inaonesha baadhi ya matini za kiutamaduni ambazo zilibainika kuwa na dhima tofauti katika lugha za kienyeji na kutafsiriwa kwa kisawe kimoja katika Kiswahili. Kwa mfano, neno ‘mtungi’ kwa Wasukuma ni kifaa kinachotumika kupikia chakula, ilhali katika jamii ya Wazanaki hutumia kuhifadhia maji ya kunywa⁵. Mfano mwingine ni ‘Kiroto’ kifaa ambacho katika

⁵ Maana na dhima ya maneno ni kwa mujibu wa waongozaji wa watalii, wahifadhi mila na wafasiri wa matini za kitalii katika Makumbusho

jamii ya Wazanaki hutumika kunywa maji. Kifaa hiki huwa na dhima sawa na neno ‘kikombe’ katika Kiswahili. Neno ‘kiroti’ kutafsiriwa kama ‘*drinking basket*’⁶ tafsiri hii haina uamilifu kwa sababu kisawe cha ‘basket’ katika Kiswahili ni ‘kikapu’.

Mfano mwingine ni neno ‘kigoda’ ambalo hurejelea kifaa chenye dhima tofauti kulingana na jamii husika. Kwa mfano, baadhi ya jamii kama vile Wahehe na Wabena hutumia kifaa hiki kama kiti cha mfalme na inapotokea akafariki, huzikwa akiwa amekaa kwenye kigoda. Hii ni tofauti na jamii ya Wanyamwezi na Wasukuma ambapo ‘kigoda’ hutumika kama kiti cha kukalia jikoni wakati mama anapopika. Vilevile, hutumika kama kiti cha tiba za asili na kiganga ambapo mgonjwa hukalia anapotibiwa na mganga⁷. Kwa hiyo, tafsiri ya ‘kigoda’ kama ‘*royal stool*’ ni tafsiri jumuishi ambayo inapoteza maana na dhima ya neno hilo katika tamaduni za jamii nyingine za Tanzania. Tatizo la kupotea kwa maana na dhima ya neno husababisha hadhira kupata maana tofauti.

Tafsiri Tofauti ya Malimwengu

Kila jamii ina uelewa tofauti wa malimwengu yake na kuyatafsiri malimwengu hayo kwa namna tofauti na jamii nyingine inavyoweza kuyaelewa na kuyatafsiri. Ilibainika kuwa, tafsiri tofauti ya malimwengu ni moja ya changamoto ya kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kwa sababu tafsiri ya Wasukuma kuhusu malimwengu yanayowazunguka ni tofauti na jinsi Wachaga wanavyoyafasili maisha yao, mazingira na uzoefu wao. Tatizo hili husababisha mfasiri kushindwa kuhamisha kwa ukamilifu maana ya majina ya jamii zaidi ya moja kwa kutumia Kiswahili. Pia, changamoto hii husababisha mtafsiri kuzalisha tafsiri kengefu kwa sababu ya kushindwa kubaini tofauti ya tafsiri ya malimwengu ya jamii lugha anazozifanyia tafsiri.

Tatizo hili lilijidhihirisha katika tafsiri ya majina ya vyakula. Kwa mfano, ilielezwa kuwa kulingana na muktadha na mazingira ya kijiografia ya jamii za Tanzania, majina ya vyakula hutolewa kulingana na dhima yake katika jamii. Mathalani, neno ‘ndizi’, katika jamii za Tanzania hupewa majina mbalimbali kulingana na aina ya ndizi, namna ya upishi, dhima na ladha yake katika jamii za

⁶ Baadhi ya tafsiri katika data zetu zilionekana kukosa uamilifu kwa sababu; wafasiri kukosa ufahamu na uelewa wa lugha zote mbili (lugha chanzi na lugha lengwa), kutokuwa makini na uteuzi wa visawe muafaka vya maneno ya utamaduni wa lugha chanzi katika utamaduni wa lugha lengwa, kutotumia kamusi kama kifaa cha tafsiri.

⁷ Maelezo haya yalitolewa na wahifadhi mila na waongozaji wa watalii wakati wa usaili katika Makumbusho zilizotembelewa

Wasafwa, Wachaga na Wahaya⁸. Hata hivyo, inapofika katika tafsiri neno ‘ndizi’ hutafsiriwa kwa kutumia kisawe kimoja tu ‘ndizi’ na inatafsiriwa kwa Kiingereza huwa ‘banana’. Katika mkabala huo, maana na dhima ya chakula hicho katika utamaduni wa lugha chanzi hupotea.

Wasafwa kwa mfano, huwa na majina tofauti ya ndizi kulingana na mazingira na tafsiri ya mazingira yao. Kwanza, kuna ndizi ziiitwazo ‘ndyali’ ambazo ni ndizi za rangi ya kijani na huliwa kama tunda. Pili, ni ‘Kambani’ ambayo ni aina nyingine ya ndizi za njano hujulikana kama ndizi kisukari. Tatu kuna ‘amatoke’, hizi ni ndizi za kupika. Kwa hiyo, katika jamii hiyo ndizi huweza kutofautishwa kulingana na aina na dhima yake. Tafsiri hii ya ndizi inaweza kuwa tofauti na jinsi jamii nyingine ambayo haina ‘ndizi’ inavyoweza kutafsiri ndizi. Kwa upande wa jamii ya Wachaga, wao pia huwa na aina tofauti za ndizi. Kwa mfano, ‘ndizi ng’ombe’ (hutumika kama chakula), ‘ndizi mshale’ (hutumika kama chakula), ‘ndizi kimalindi’ (hutumika kama chakula na tunda), ‘ndizi kitarasa’ (hutumika kama chakula), ‘ndizi kibungala’ (hutumika kutengenezea Mbege), ‘ndizi mtoto’ (hutumika kutengenezea Mbege), ‘ndizi mkonozi’ (hupikwa chakula kijulikanacho kama kiburu). Kwa hiyo, ukichunguza majina ya ndizi katika jamii hizo yanatofautiana kulingana na jamii husika. Aidha, kila aina ya ndizi hutumika kulingana na dhima yake katika utamaduni wa jamii hiyo. Kwa hiyo, kutafsiri ‘ndizi’ kama ‘ndizi’ na hatimaye ‘banana’ hupoteza maana na dhima za kiutamaduni za neno hilo katika jamii.

Matumizi ya Neno Moja Kurejelea Maneno zaidi ya Moja

Ilielezwa wakati wa usaili kuwa, changamoto ya kutafsiri matini za kiutamaduni husababishwa na matumizi ya neno moja la Kiswahili kutumika kama kisawe cha maneno zaidi katika kijamii. Tatizo hili huyafanya baadhi ya maneno kuwa na maana tata na hatimaye kupoteza maana. Kwa mfano, wakati wa usaili na katika dodoso wahojiwa walitaja baadhi ya maneno ambayo yalionekana kutafsiriwa kwa kutumia kisawe kimoja wakati yakiwa na dhana tofauti. Kwa mfano, majina ya vifaa kama vile ‘chungu’, ‘kibuyu’, ‘kigoda’, ‘ungo’, ‘mtungi’n.k. huwakilishwa na majina tofauti kulingana na dhima yake ndani ya jamii. Kwa upande mwingine, katika Kiswahili maneno hayo huwakilishwa kwa kisawe kimoja. Kwa jinsi hiyo maana iliyokusudiwa hupotea. Tazama mifano ifuatayo:

⁸ Wasafa ni jamii lugha ya Tanzania iishiyo katika mkoa wa Mbeya; Wachaga ni jamii lugha ya Tanzania inayopatikana mkoa wa Kilimanjaro na Wahaya ni jamii lugha ya Tanzania inayopatikana mkoa wa Kagera

Jedwali Na. 3: Tafsiri ya Vinywaji

| Jamii Lugha | Jina katika lugha ya kijamii (MC) | Tafsiri ya Kiswahili (ML1) | Tafsiri ya Kiingereza (ML2) |
|-------------|-----------------------------------|----------------------------|-----------------------------|
| Wachaga | Mbege | Mbege | <i>Local beer</i> |
| Wafipa | Kimpumu | Kimpumu | <i>Local beer</i> |
| Wahaya | Lubisi | Lubisi | <i>Local beer</i> |
| Wazanaki | Amarwa | Amarwa | <i>Local beer</i> |

Chanzo: Matini za Kitalii za Makumbusho

Jedwali Na. 3 hapo juu, linaonesha kuwa tafsiri ya majina ya vinywaji katika jamii ulumbi huhawilishwa kama yalivyo kutoka lugha ya kikabila hadi Kiswahili. Pia, huhawilishwa kwa kutumia kisawe jumuishi katika lugha ya Kiingereza.

Eneo la Jamii Ulumbi kuwa Kikwazo cha Mawasiliano

Eneo la jamii ulumbi huwa na utamaduni changamani. Utamaduni huo huwasilishwa kwa kutumia lugha ya kitaifa ambayo ndiyo lugha inayounganisha lugha zote ndani ya jamii ulumbi. Aidha, lugha ya kitaifa hushindwa kufumbata uchangamani wa kiutamaduni na kubeba mzigo wa tamaduni zaidi ya moja. Mzigo huo husababisha kupotea kwa baadhi ya tamaduni za jamii na hivyo kuzalisha tafsiri iliyokengeuka. Kwa mfano, neno ‘chungu’ katika jamii za Tanzania hutofautiana kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Neno hili, huwa na dhima tofauti kutegemea utamaduni. Data za utafiti huu zinadhihirisha kuwa, wakati wa kutafsiri neno ‘chungu’ katika jamii lugha za Tanzania, neno hilo hubeba maana na dhima ya neno hilo katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa TUKI (2014), chungu ni chombo kilichofinyangwa kwa udongo na kitumiwacho kupikia. Kwa kiwango fulani, maelezo haya yanaweza kuleta utata kwa kuwasi jamii zote hutumia ‘chungu’ kama kifaa cha kupikia. Tazama jedwali lifuatalo linaloonesha dhima ya chungu katika baadhi ya lugha za kijamii⁹.

⁹ Dhima hizi ni kulingana na wahifadhi mila na waongozaji wa watalii katika Makumbusho zilizotembelewa

Jedwali Na. 4. Dhima ya ‘chungu’ katika jamii lugha za Tanzania


| Jamii lugha | Dhima ya chungu |
|--------------------|--|
| Wasukuma | <i>Nungu</i> Kupikia na kuhifadhia maji |
| Wabena | <i>Hiviya</i> kupikia, pambo, kuhifadhia mazao, kuboresha muziki na kunywea maji |
| Wanyakyusa | <i>Indeko</i> (chungu kidogo) kupikia <i>Isyala</i> (chungu kikubwa) kuhifadhia maji ya kunywa, kuhifadhia unga, kuhifadhia pombe na kuhifadhia mazao |
| Wagogo | <i>Nyunguu</i> kupikia chakula Njiloo kuhifadhia maji ya kunywa |
| Wapare | <i>Nyungu</i> kuhifadhia maji, kupikia na hutumika kuwekea zawadi za bibi harusi siku ya harusi |

Chanzo: Matini za Kitalii za Makumbusho

Katika jedwali Na. 3 neno ‘chungu’ linadhihirisha maana na dhima tofauti tofauti katika jamii lugha nchini Tanzania. Kwa hiyo, kutozingatia dhima za kiutamaduni za vifaa vya jamii katika jamii ulumbi ni changamoto ambayo husababisha kupotea kwa maana iliyokusudiwa.

Mchakato wa Kutafsiri Matini za Kiutamaduni

Baada ya kuchunguza matini za kitalii na matokeo ya data za usaili pamoja na dodoso, makala haya yalibaini kuwa, mkakati wa kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi huanzia lugha za kienyeji na kisha kutafsiriwa hadi Kiswahili na hatimaye lugha ya Kiingereza. Hatua hii inadhihirisha kuwa, tafsiri ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi hupitia mchakato maalumu kama unavyodhihirika katika kielelezo kifuatacho:



Ufunguo:

1. Uhusiano kapa
2. Uhusiano pacha
3. Hatua za tafsiri
4. Uhusiano wa moja kwa moja
5. Uhusiano usio wa moja kwa moja
6. Uhusiano wa moja kwa moja

Kielelezo Na. 1 Mchakato wa Kutafsiri Matini za Kiutamaduni katika Utalii
Chanzo: Matini za Kitalii za Makumbusho

Kielelezo Na.1, kinaonesha hatua za mchakato wa kutafsiri matini za kiutamaduni. Kulingana na kielelezo hicho, inabainika kuwa, mchakato wa kutafsiri matini za kiutamaduni hupitia hatua tatu: kwanza ni lugha za kijamii, hatua ya pili ni lugha ya Kiswahili na hatua ya tatu ni Kiingereza.

Kulingana na Kielelezo Na. 1, matini chanzi huwa ni matini za lugha za kienyeji. Tafsiri huanzia matini chanzi (MC- lugha za kienyeji) hadi matini lengwa (ML1) ambayo ni Kiswahili. Katika hatua ya pili, mchakato wa tafsiri hufanyika kutoka matini lengwa 1 (ML1 - Kiswahili) kwenda matini lengwa (ML2) ambayo ni Kiingereza. Hivyo basi, kielelezo hicho kinaonesha kuwa mchakato wa kutafsiri matini za kitalii hupitia hatua tatu na hupitia katika madaraja mawili ya mchakato wa tafsiri.

Uhawilishaji wa ujumbe na tafsiri yake hujikita katika mahusiano. Inaonesha kuwa, kuna mahusiano pacha ya tafsiri ya ujumbe baina ya MC na ML1. Uhusiano huu unatokana na ukaribu wa kiisimu, sifa za kiisimu, kihistoria, kijiografia na kimazingira kati ya MC na ML1. Lugha ya Kiswahili pamoja na baadhi ya lugha za

kijamii zina asili ya Kibantu. Uhusiano huu huzifanya lugha hizi kuwa na ukaribu wa kiisimu na kufanya kuwepo na mahusiano pacha katika ufahamu na utambuzi wa ujumbe kwa hadhira.

Sifa za kiisimu kama vile muundo, maumbo na mpangilio wa maneno katika lugha ya Kiswahili huwa sawa na lugha nyingine za Kibantu. Lugha hizo za kijamii pamoja na Kiswahili, huwa katika mazingira sawa ya kijiografia, kiuchumi, kiitikadi, na kihistoria. Hivyo basi, tofauti zake huwa ni ndogo katika urejelezi wa maana ya maneno tofauti na lugha ya Kiingereza ambayo ina uhusiano wa mbali kiisimu na kiutamaduni dhidi ya lugha za Kibantu.

Kwa upande mwingine, tunaona kuwa, kuna uhusiano kapa baina ya MC na ML2. Yaani, kuna uhusiano kapa baina ya UL2, UC na UL1. Pia, kuna uhusiano kapa wa lugha lengwa 2 (LL2) na lugha lengwa 1 (LL1) pamoja na lugha chanzi (LC). Aidha, kuna uhusiano usio wa moja kwa moja baina ya matini chanzi na matini lengwa 2. Hivyo basi, mahusiano haya hutokana na sababu za mwachano wa lugha husika katika misingi ya kiisimu, kijiografia, kihistoria, wakati na muktadha. Jilala (2014) anajadili kuwa, lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili zina mwachano mkubwa wa kiisimu na kiutamaduni. Kwa hiyo, tafsiri ya matini ya kiutamaduni katika lugha hizi huwa ni zoezi gumu. Aidha, tofauti ya hatua za maendeleo baina ya jamii ya lugha hizi husababisha kuwepo kwa mahusiano kapa na mahusiano yasiyo ya moja kwa moja. Malangwa (2010) anadai kuwa lugha ya Kiingereza imepiga hatua katika maendeleo ya sayansi na teknolojia na hivyo ina msamiati wa kutosha. Kwa maana hiyo, hatua hizi za kimaendeleo husababisha tofauti katika utamaduni wa jamii. Kielelezo Na.1 kinadhihirisha kuwa, kila lugha ina utamaduni wake ambao ni tofauti na utamaduni wa lugha nyingine. Tofauti hizi huweza kuathiri tafsiri ya maana na ujumbe wa majina au maneno yaliyofungamana na utamaduni. Kwa hiyo, katika jamii ulumbi mfasiri anatakiwa kubaini tofauti za kiutamaduni za lugha zinazounda jamii ulumbi ili aweze kuzifumbata wakati wa kutafsiri matini za kiutamaduni.

Mapendekezo

Makala haya yalilenga kutoa mapendekezo ya namna ya kuzikabili matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi. Kwa hiyo, baada ya kuchunguza na kujadili changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi na mchakato wa kutafsiri majina hayo, swali la kujiuliza lilikuwa ni: nini kifanyike kuboresha mkakati wa kuzikabili matini za kiutamaduni hususan majina katika jamii ulumbi? Wakati wa mahojiano na wahifadhi mila, wafasili wa matini za kitalii na waongozaji wa watalii, makala hii ilibaini kuwa zipo njia zinazoweza kutumika kuzikabili matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi. Sehemu hii inatoa mapendekezo ya namna mchakato wa kutafsiri majina ya kiutamaduni unavyoweza kufanyika ili kufumbata maana na ujumbe wa majina katika jamii ulumbi.

Usawazishaji wa Istilahi za Kiutamaduni

Kutokana na data zilizopatikana katika utafiti huu pamoja na mjadala wa makala haya, makala yanapendekeza kuwepo kwa mkakati wa kusawazisha istilahi za kiutamaduni ili kuwa na uwiano wa maana na ujumbe wa matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi. Kufanya hivyo, kutasaidia katika kuunda istilahi za kiutamaduni ambazo zinawakilisha utamaduni wa kitaifa katika jamii ulumbi. Jambo hili litasaidia kuondoa matatizo ya mawasiliano baina ya hadhira chanzi na hadhira lengwa na kuondoa utata wa maana na ujumbe. Usawazishaji wa istilahi za kiutamaduni una changamoto zake ambazo ni pamoja na mchakato huu kuhitaji gharama, muda, fedha, na kufanya utafiti na makubaliano ya jamii zote kuhusu istilahi za msingi za kiutamaduni katika jamii yote.

Ufahamu wa Utamaduni wa Jamii

Ufahamu na uelewa wa utamaduni wa jamii ni jambo la msingi kwa mfasiri wa matini ya aina yoyote. Makala haya yanapendekeza kuwa, mfasiri anatakiwa kuwa na ufahamu na uelewa wa utamaduni wa jamii zote mbili yaani; jamii chanzi na jamii lengwa. Kwa hiyo, kuelewa utamaduni wa jamii hizo kutasaidia katika kuelewa tofauti za kiutamaduni na namna ya kuzikabili wakati wa kutafsiri matini za aina hiyo. Kwa mfano, kwa kuelewa kuwa neno ‘nyungu’ kwa Mpare lina dhima zaidi ya moja itamsaidia mfasiri kutofautisha ‘nyungu’ ya Mpare na ‘nungu’ ya Msukuma na kuziweka wazi tofauti hizi wakati wa kutafsiri matini hizo. Vilevile, mfasiri anatakiwa kuelewa maana ya majina yaliyofungamana na utamaduni wa jamii ili kutumia muktadha wa utamaduni mahususi katika kutafsiri. Uelewa huu utamsaidia mfasiri kuepuka utata na upotoshaji wa maana.

Uzingativu wa Mbinu mwafaka katika Tafsiri

Tafsiri kama mchakato unahitaji kuwepo na mbinu mwafaka ili kufikia lengo la mchakato huo. Kwa hiyo, makala haya yanapendekeza mfasiri wa matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kuzingatia uteuzi na matumizi ya mbinu mwafaka za tafsiri ili kuzalisha matini bora. Kwa mfano, wakati wa uhawilishaji wa matini za kitalii anaweza kutumia mbinu ambayo itaziingiza maana na dhima za kiutamaduni katika tafsiri ili kuziweka bayana kwa hadhira. Mbinu ambayo itamsaidia kutoa ufafanuzi wa maana za ziada katika matini za kiutamaduni ili kuwasaidia hadhira kuelewa maana lengwa bila taklifu.

Mbinu inayoweza kufumbata maana, ujumbe na dhima ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kama vile, matumizi ya mbinu ya uasilishaji na ufafanuzi wa visawe inaweza kusaidia kuweka bayana maana na dhima za kiutamaduni. Jambo hili litasaidia katika kukabili changamoto la ukosefu wa visawe kwa kutoa ufafanuzi wa maneno ambayo hayana visawe vyake katika lugha ya Kiswahili. Kama tulivyoona hapo awali, lengo la kutafsiri matini za kiutamaduni ni kuutambulisha utamaduni wa jamii. Hivyo, tafsiri lazima ikidhi lengo hilo kwa kuzingatia mbinu na hatua madhubuti za tafsiri.

Uzingativu wa Hatua za Tafsiri

Makala haya yanapendekeza uzingativu wa hatua madhubuti na mikakati mahususi katika kutafsiri matini za kiutamaduni. Jilala (2014) katika Modeli ya Mawasiliano ya Kiutamaduni (MMK) amependekeza hatua tano za kutafsiri matini za kiutamaduni. Hatua hizo ni; maandalizi, utafutaji wa visawe vya kiutamaduni, mchakato wa tafsiri, uhusiano na uzalishaji wa matini lengwa. Kwa hiyo, hatua hizi zinaweza kumwongoza mfasiri kuzalisha matini bora endapo atazitumia ipasavyo.

Kuzingatia Tofauti za Kiutamaduni

Mfasiri anapaswa pia kuelewa kuwa kila jamii ina utamaduni wake. Kwa hiyo, ni muhimu kuzishughulikia tofauti hizo wakati wa kutafsiri matini za kiutamaduni ili kujiepusha na uzalishaji wa tafsiri kengeufu. Data za makala haya zimedhihirisha kuwa, tofauti za kiutamaduni huathiri tafsiri ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi. Kwa hiyo, ili kukabiliana na tatizo hilo, mfasiri anapaswa kuelewa tamaduni za jamii anazozifanyia kazi.

Hitimisho

Makala haya yamejadili kwa kina changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kwa kutumia mifano ya majina katika matini za kitalii nchini Tanzania. Mjadala wa makala haya unasisitiza kuwa, katika jamii ulumbi kuna utamaduni changamani ambao hukusanya tamaduni za jamii zaidi ya moja. Kimsingi, changamoto zilizobainishwa katika makala haya ni za kisemantiki, ukosefu wa visawe vya Kiswahili, tofauti ya dhima ya maneno, tafsiri tofauti ya malimwengu, matumizi ya neno moja kurejelea maana zaidi ya moja, eneo la jamii ulumbi kuwa kikwazo cha mawasiliano na muingiliano wa tamaduni.

Aidha, makala haya yamepambanua kuwa mchakato wa kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi ni mchakato ambao hupitia hatua tatu. Hatua ya lugha za kijamii, lugha ya Kiswahili pamoja na ya Kiingereza. Mchakato huu unaifanya tafsiri ya matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi kuwa ni 'tafsiri ya tafsiri'. Pia makala haya yanajadili kuwa, wakati wa kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi, lugha kuu hubeba mzungo katika kufumbata tamaduni zote na kuziwasilisha kama utamaduni wa jamii moja. Kushindwa kubeba mzungo huu husababisha kuzalisha tafsiri zenye ukinzani wa maana na ujumbe na hata kupoteza ujumbe chanzi. Kwa hiyo, makala haya yanapendekeza kuwa ili kukabiliana na changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ulumbi ni muhimu kuwepo na usawazishaji wa istilahi za kiutamaduni, uzingativu wa mbinu mwafaka za tafsiri, ufahamu wa utamaduni wa jamii zote pamoja na uzingativu wa hatua za tafsiri.

Marejeleo

- Baker, M. (1992). *In Other Words: A Course Book on Translation*. London: Routledge Print.
- Gentzler, E. (2001). *Contemporary Translation Theories*. London and New York: Routledge.
- Iser, W. (1978). *The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response*. Baltimore MD: The Johns Hopkins University Press.
- Jilala, H. (2014a). Athari za Kiutamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka Matini za Kitalii katika Makumbusho za Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (hajichapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Jilala, H. (2014 b). Matatizo ya Tafsiri katika Matini Nchini Tanzania. Katika kioo cha lugha.
- Omari S na Peterson (wah.) Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Juz. No.12 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk. 27-47.
- Katani, D. (2004). *Translating Cultures: An Introduction for Translators, Interpreters and Mediators. (Toleo la 2)*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Lauscher, S. (2000). Translation Quality Assessment: Where can Theory and Practice meet? *The Translator*, Juzuu Na. 6, (2), uk.149-168.
- LOT (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Malangwa, S. P. (2010). "Handling Technical Translations: The Case of Translation of *Computer Programs from English into Kiswahili*." Tasnifu ya Uzamivu (Haijichapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Manyasa, J. (2008). "Investigating The Basis of Naming People in Kisukuma" Tasnifu ya Umahiri (Haijichapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Msanjila, Y. P. (1997). Towards A Policy on The Use of Kiswahili in Africa, katika *Kiswahili*. Vol. 60, uk. 61-67. Dar es Salaam: TUKI
- Msanjila Y.P, Kihore. Y. M na Masamba, B. P. D. (2009). *Isimu Jamii Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

- Mtesigwa C.K. (2004). Utandawazi na Dhima ya Kiswahili katika *Kiswahili na Utandawazi*: Makala ya siku ya Kiswahili. Dar es Salaam. Uk.18-33.
- Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nida, E. A. (2001). *Language and Culture: Context in Translating*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Ed Press.
- Nord, C. (1991). Skopos, Loyalty and Translational Conventions. *Target*, 3 (1), uk. 91-109
- Nord, C. (1997). *Translating as A Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome.
- Nord, C. (2001). *Translating as A Purposeful Activity: Functionalist Approaches Explained*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Nord, C. (2005). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology and Didactic Application of A Model for Translation-Oriented Text Analysis*. (toleo la 2). New Jersey: Rodopi B.V. Amsterdam-New York.
- Ndlovu, V. (2000). Translating Aspect of Culture in 'Cry, The Beloved Country' in Zulu; *Language Matter*, Juzuu Na. 31 (1), uk. 72-102.
- Reiss, K. na Vermeer, H. (1994). *Groundwork for a General Theory of Translation*. Tübingen: Niemeyer.
- Rubanza, Y. I. (2000). "The Linguistics Creativity of Haya Personal Names" in *Kiswahili*, Vol. 63
- Rugemalira, J. (2005). *A Grammar of Runyambo*, Dar es salaam, Language Project University of Dar es Salaam.
- Ryanga, S.C.W.A. (2004). Matumizi ya Kiswahili katika Diplomasia katika *Kiswahili na Utandawazi*: Makala ya siku ya Kiswahili. Dar es Salaam. Uk. 107-126.
- Sewangi S. S. (2004). Mchango wa Intaneti katika Ukuzaji wa Kiswahili katika *Kiswahili na Utandawazi*: Makala ya siku ya Kiswahili. Dar es Salaam. Uk.45-51.

- TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la 3. TATAKI. Oxford University Press.
- Vermeer, H. (1987). What does It mean to Translate? Katika *Indian Journal of Applied Linguistics* Juzuu Na. 13 (2), uk. 25-33.
- Vermeer, H. (1989). Skopos and Commission in Translation Action. Katika A. Chesterman (Mh.). *Readings in Translation Theory*. Oy Finn Lectura Ab, uk.173-187.
- Vermeer, H. (1994). Translation Today: Old and New Problems. Katika M. S. Hornby (Mh), *Translation Studies: An Interdiscipline*. Philadelphia: John Benjamins.
- Vermeer, H. (1999). *A Skopos Theory of Translation*. Heidelberg: Textcon Text.
- Vermeer, H. (2000). Skopos and Commission in Translation Action. Katika L. Venuti, (Mh.), *The Translation Studies Reader*. New York: Routledge, uk. 227-237.